JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# FOMATI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI

**IMETOLEWA NA:**

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
S.L.P 2624
**DAR ES SALAAM**
**TANZANIA**

**Imeboreshwa**
**JANUARI, 2024**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# FOMATI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI

**IMETOLEWA NA:**

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
S.L.P 2624
**DAR ES SALAAM**
**TANZANIA**

**Imeboreshwa**
**JANUARI, 2024**

Imechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2024

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........................................................................................................ iv

01 KISWAHILI ........................................................................................................ 1

02 ENGLISH LANGUAGE ........................................................................................................ 5

03 MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI ........................................................................................................ 8

04 HISABATI ........................................................................................................ 13

05 SAYANSI NA TEKNOLOJIA ........................................................................................................ 17

06 URAIA NA MAADILI ........................................................................................................ 20

## DIBAJI

Kitabu hiki cha fomati ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kimeandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania kwa kuzingatia matakwa ya Mtaala wa Elimu ya Msingi wa mwaka 2015. Fomati hii itaanza kutumika mwaka 2024.

Katika kitabu hiki cha Fomati kuna maboresho ya idadi ya sehemu za karatasi hususani katika masomo ya **03 Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi, 04 Hisabati**, **05 Sayansi na Teknolojia** na **06 Uraia na Maadili** ambapo kutakuwa na sehemu **tatu (03)** A, B na C badala ya **mbili (2)** za awali ambazo ni A na B. Maboresho zaidi yaliyofanyika katika muundo wa mtihani wa masomo yote yanayotahiniwa katika ngazi hii ya elimu ambayo ni **01 Kiswahili**, **02 English Language**, **03 Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi, 04 Hisabati**, **05 Sayansi na Teknolojia** pamoja na **06 Uraia na Maadili**. Muundo wa Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi utakuwa na idadi ya maswali ambayo ni tofauti kutoka somo moja hadi jingine ikilinganishwa na idadi ya awali ambapo masomo yote yalikuwa na maswali 45. Katika maboresho hayo masomo ya **01 Kiswahili** na **06 Uraia na Maadili** yatakuwa na maswali **sita (6)** kila moja. Masomo ya **04 Hisabati** na **05 Sayansi na Teknolojia** yatakuwa na maswali **nane (8)** kila moja. Aidha, masomo ya **02 English Language** na **03 Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi** yatakuwa na maswali **saba (7)** kila moja. Katika mitihani hiyo mtahiniwa ataandika majibu yake kwenye nafasi zilizotengwa katika karatasi ya maswali.

Fomati za mtihani zimeandaliwa kwa kufuata muundo wa sehemu tano ambazo ni Utangulizi, Malengo ya Jumla, Umahiri Mkuu, Muundo wa Mtihani na Umahiri utakaotahiniwa kwa kila somo. Aidha, Jedwali la utahini limewekwa mwishoni mwa fomati ya kila somo na linaonesha umahiri utakaopimwa, ngazi za nyanja ya utambuzi, idadi ya vipengele vya maswali kwa kila umahiri mahususi na asilimia ya uzito kwa kila umahiri.

Kwa ujumla, kitabu hiki cha fomati kinatoa mwongozo kwa watunzi wa mitihani, warekebishaji wa maswali ya mtihani na walimu wa shule za msingi katika kuandaa mitihani inayozingatia haki, uhalali na viwango. Baraza linasisitiza umahiri wote katika masomo yote yanayofundishwa katika ngazi ya elimu ya msingi ufundishwe kwa kuzingatia mihtasari ya masomo husika. Fomati hii ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa namna yoyote ile **isitumike** kama mbadala wa mihtasari ya masomo husika.

Baraza la Mitihani linatambua na kuthamini mchango wa watu wote walioshiriki katika kufanya maboresho ya kitabu hiki cha fomati.

Dkt. Said Ally Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

# 01 KISWAHILI

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi somo la Kiswahili imeandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo la Kiswahili wa mwaka 2015 ulioanza kutumika 2017 (toleo la 2019). Muhtasari huo unabainisha Umahiri Mkuu na umahiri mahususi ambao mwanafunzi anatakiwa kuupata katika ngazi ya Elimu ya Msingi Darasa la III hadi VII. Hivyo, mtihani wa somo la Kiswahili utakaoandaliwa kwa kutumia fomati hii, utalenga kupima umahiri alioupata mtahiniwa kuanzia Darasa la III hadi VII.

Fomati hii ni zao la maboresho yaliyofanyika kutoka fomati ya mwaka 2020 ambayo ilikuwa na maswali **45**. Hivyo, mtihani wa somo la **Kiswahili** utakuwa na maswali **sita (6)** yenye jumla ya vipengele **35** ambavyo vimetoka katika umahiri mahususi wa aina **sita (6)** katika umahiri mkuu wa aina **mbili (2)**. Lengo la maboresho haya ni kumwezesha mtahiniwa kuendana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia yanayotokea duniani kote na ujenzi wa msingi wa umahiri katika masomo ya sekondari na elimu ya juu.

## 2.0 MALENGO YA JUMLA

Mtihani wa somo la Kiswahili utapima ni kwa kiwango gani mtahiniwa anaweza:

2.1 Kusikiliza, kusoma na kuandika kwa kutumia lugha ya Kiswahili;

2.2 Kutumia Kiswahili fasaha katika miktadha mbalimbali;

2.3 Kutumia Kiswahili kupata maarifa, stadi na mwelekeo wa kijamii, kiutamaduni, kiteknolojia na kitaaluma kutoka ndani na nje ya nchi;

2.4 Kukuza stadi za mawasiliano ili kumwezesha mwanafunzi kumudu maisha yake;

2.5 Kujenga msingi bora na imara wa kujifunza kwa ajili ya elimu ya juu na kujiendeleza binafsi kwa kutumia lugha ya Kiswahili; na

2.6 Kuifahamu na kuitumia lugha ya Taifa.

## 3.0 UMAHIRI MKUU

Mtihani utapima ujuzi na utendaji wa mtahiniwa katika:

3.1 Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali; na

3.2 Kuonesha uelewa wa jambo alilosikiliza au kulisoma.

## 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

Mtihani wa somo la Kiswahili utakuwa na karatasi **moja (1)** na utafanyika kwa muda wa **saa 1:40** kwa watahiniwa wote isipokuwa kwa watahiniwa wenye mahitaji maalum ambapo mtihani wao utafanyika kwa **saa 1:55**. Mtihani utakuwa na sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **sita (6)** yenye jumla ya vipengele **35**. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote** yenye jumla ya alama **50**.

**Sehemu A** itakuwa na maswali **matatu (3)**. Swali la kwanza na la pili yatakuwa ya kuchagua jibu sahihi na swali la tatu litakuwa la kuoanisha. Swali la kwanza litakuwa na vipengele **vitano (5)** vitakavyotokana na kifungu cha maneno/hadithi itakayosomwa na Msimamizi ambapo mtahiniwa atatakiwa kusikiliza kwa makini kisha kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguo. Swali la pili litakuwa na vipengele **10** ambapo mtahiniwa anatakiwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguo **A - E**. Swali la tatu litakuwa na vipengele **vitano (5**) vya kuoanisha. Kila kipengele katika sehemu hii kitakuwa na alama **moja (1)** hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama **20**.

**Sehemu B** itakuwa na maswali **mawili (2)** ambayo ni swali la nne na la tano. Swali la nne litakuwa na vipengele **vitano (5)** ambapo mtahiniwa atatakiwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi au kupanga sentensi katika mtiririko unaoleta mantiki na kuunda kifungu cha habari. Swali la tano litakuwa la majibu mafupi lenye vipengele **vitano (5)** kutoka katika kifungu cha habari, hadithi au shairi. Kila kipengele kitakuwa na alama **mbili (2)**. Hivyo, sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **20**.

**Sehemu C** itakuwa na swali **moja (1)** la utungaji lenye vipengele **vitano (5)** vyenye jumla ya alama **10**.

## 5.0 UMAHIRI UTAKAOTAHINIWA

Umahiri utakaotahiniwa katika mtihani wa Kiswahili ni kama ifuatavyo:

5.1 Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali;

5.2 Kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali;

5.3 Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali;

5.4 Kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza;

5.5 Kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma; na

5.6 Kutumia msamiati katika kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali.

**Jedwali la Utahini Somo la 01 Kiswahili**

| Na. | UMAHIRI MAHUSUSI | NGAZI ZA NYANJA YA UTAMBUZI ZITAKAZOPIMWA | | | | | | Idadi ya Vipengele vya Maswali kwa kila Umahiri | Asilimia ya uzito kwa kila Umahiri |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kukumbuka | Kuelewa | Kutumia | Kuchambua | Kutathmini | Kuunda | | |
| 1. | Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali. | | | | | | | 10 | 28.5 |
| 2. | Kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali. | | | | | | | 5 | 14.3 |
| 3. | Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali. | | | | | | | 5 | 14.3 |
| 4. | Kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza. | | | | | | | 5 | 14.3 |

| Na. | UMAHIRI MAHUSUSI | NGAZI ZA NYANJA YA UTAMBUZI ZITAKAZOPIMWA | | | | | | Idadi ya Vipengele vya Maswali kwa kila Umahiri | Asilimia ya uzito kwa kila Umahiri |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kukumbuka | Kuelewa | Kutumia | Kuchambua | Kutathmini | Kuunda | | |
| 5. | Kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma. | | | | | | | 5 | 14.3 |
| 6. | Kutumia msamiati katika kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali. | | | | | | | 5 | 14.3 |
| **Idadi ya Vipengele vya Maswali** | | | | | | | | **35** | |
| **Asilimia ya Uzito wa Vipengele vya Maswali kwa kila Ngazi ya Utambuzi** | | | | | | | | | **100** |

## 02 ENGLISH LANGUAGE

### 1.0 INTRODUCTION

This revised Primary School Leaving Examination format for English Language subject is based on the 2015 English Language Syllabus for teaching standards III to VII which was effectively used in 2017 (revised in 2019). That syllabus outlines the general and specific competencies that pupils ought to acquire at the primary education level from standard III to VII. As such, the English Language examination will assess the competencies each candidate had acquired from standard III to VII.

The revised format replaces the 2020 English Language format which had consisted of **45** questions. This format, on the other hand, will have **7** questions with **35** assessment items for all four specific competencies derived from three general ones. These improvements aim at enabling a candidate to cope with the development of Science and Technology, which takes place in the contemporary world and build a competency foundation for secondary and higher education.

### 2.0 GENERAL OBJECTIVES

The English Language examination aims to test the candidate's ability to:

2.1 Express him/herself appropriately in a given situation;
2.2 Use basic skills in listening, reading and writing in English;
2.3 Use vocabulary through listening, reading, and writing;
2.4 Apply correct English grammar; and
2.5 Use the English Language in acquiring higher education and for personal advancement.

### 3.0 GENERAL COMPETENCIES

The examination will measure the candidate's competencies in how to:

3.1 Comprehend oral and written information,
3.2 Communicate through writing, and
3.3 Use vocabulary through listening, reading and writing.

### 4.0 EXAMINATION RUBRIC

The examination will consist of **one (1)** paper of **1:40 hours**. The paper for the candidates with special needs will last for **1:55 hours**. This paper will comprise three sections, A, B and C, and will have

**seven (7)** questions with **35** items. The candidates must answer **all** the questions, which account for **50** marks.

**Section A** will consist of **four (4)** questions. The first question will be based on a passage/story which the invigilator will read out aloud to the candidates. A candidate should listen attentively to the passage and respond, accordingly, to **five (5)** multiple choice items. The second question will consist of **five (5)** short answer items that require the candidates to choose the correct answer from options A - E. The third question will require the candidates to complete **five (5)** sentences (i-v) by writing down the correct words picked from the options provided. The fourth question will contain **five (5)** matching items. Each item in this section will carry **one (1)** mark. This section will weigh **20** marks.

**Section B** will consist of **two (2)** questions (Question 5 and 6), each with **five (5)** items. The fifth question with five items will require candidates to fill in the blank spaces. The sixth question with **five (5)** items will require candidates to read and understand the written information and, accordingly, respond to **five (5)** short answer items. Each item will carry **two (2)** marks. The section will weigh a total of **20** marks.

**Section C** will consist of **one (1)** question with five items on arranging the jumbled sentences logically or writing a composition. Each item will carry **two (2)** marks. The section will account for **10** marks.

## 5.0 ASSESSMENT COMPETENCIES

The following competencies will be assessed:

5.1 Listening and understanding information presented orally;
5.2 Developing and using vocabulary appropriately through listening, writing and reading;
5.3 Communicating simple ideas through writing; and
5.4 Reading and comprehending written information.

## Table of Specifications for 02 English Language Subject

| S/N | SPECIFIC COMPETENCES | COGNITIVE LEVELS TO BE TESTED | | | | | | Number of Items per Competence | Percentage Weighting per Competence |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Remembering | Understanding | Applying | Analysing | Evaluating | Creating | | |
| 1. | Listening and comprehending information presented orally. | | | | | | | 5 | 14.3 |
| 2. | Developing and using vocabulary Appropriately through listening, writing and reading. | | | | | | | 10 | 28.6 |
| 3. | Communicating simple ideas through writing. | | | | | | | 15 | 42.8 |
| 4. | Reading and comprehending written information. | | | | | | | 5 | 14.3 |
| **Total Number of Items per Cognitive Level** | | | | | | | | **35** | **100** |
| **Total Percentage weight of Items per Cognitive Level** | | | | | | | | | |

## 03 MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi katika somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi imeandaliwa kwa kuzingatia Muhtasari wa somo hilo wa mwaka 2015 ulioanza kutumika 2017 (toleo la 2019). Muhtasari huo umebainisha Umahiri Mkuu na Umahiri Mahsusi ambao mwanafunzi anatakiwa kuupata katika ngazi ya Elimu ya Msingi Darasa la III hadi VII. Hivyo, mtihani wa somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi utakaoandaliwa kwa kutumia fomati hii, utalenga kupima umahiri alioupata mtahiniwa kuanzia Darasa la III hadi VII.

Fomati hii ni zao la maboresho yaliyofanyika kutoka fomati ya mwaka 2020 ambayo ilikuwa na maswali **45** na imeboreshwa na kuwa na maswali **saba (7)** yenye jumla ya vipengele **35** kutoka katika umahiri mkuu wa aina zote **nane (8)**. Fomati hii pia kama ile ya awali inahusisha kumpima mtahiniwa katika ngazi zote za nyanja ya utambuzi. Lengo la maboresho haya ni kumwezesha mtahiniwa kuendana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia yanayotokea duniani kote na ujenzi wa msingi wa umahiri katika masomo ya sekondari na elimu ya juu.

## 2.0 MALENGO YA JUMLA

Mtihani wa Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi unalenga kupima ni kwa kiwango gani mtahiniwa anaweza:

2.1 Kuthamini na kulinda mazingira na rasilimali za taifa;

2.2 Kuthamini uhusiano wa watu na mazingira katika jamii;

2.3 Kutambua na kutumia fursa zilizopo katika mazingira yake;

2.4 Kutambua asili ya jamii za taifa letu;

2.5 Kujenga misingi ya kujitegemea;

2.6 Kuwa mbunifu; na

2.7 Kutambua fursa katika mazingira yake.

## 3.0 UMAHIRI MKUU

Mtihani utapima ujuzi na utendaji wa mtahiniwa katika:

3.1 Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka;

3.2 Kutambua misingi ya uzalendo katika jamii;

3.3 Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku;

3.4 Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali;

3.5 Kutumia misingi ya unadhifu;

3.6 Kumudu mapishi mbalimbali;

3.7 Kusanifu kazi za sanaa; na

3.8 Kutumia stadi za ujasiriamali.

## 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

Mtihani wa Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi utakuwa na karatasi **moja (1)** na utafanyika kwa muda wa **saa 1:30** kwa watahiniwa wote isipokuwa kwa watahiniwa wenye mahitaji maalum ambapo mtihani wao utafanyika kwa **saa 1:45**. Mtihani utakuwa na sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **saba (7)** yenye jumla ya vipengele **35**. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali yote. Jumla ya alama zitakuwa **50**.

**Sehemu A** itakuwa na maswali **mawili (2)** yenye jumla ya vipengele **20**. Swali la kwanza litakuwa la kuchagua jibu sahihi lenye vipengele **15** vinavyoundwa na machaguo matano **A**-**E**. Swali la pili litakuwa na vipengele **vitano (5)** vya kuoanisha ambapo mtahiniwa atatakiwa kuoanisha maswali katika orodha A na majibu katika orodha B au kuchagua neno au maneno ya jibu sahihi kutoka katika kisanduku na kuyaandika katika nafasi ya majibu atakayopewa. Kila kipengele kitakuwa na alama **moja (1)**, hivyo jumla ya alama katika sehemu hii itakuwa **20.**

**Sehemu B** itakuwa na maswali **manne (4)**, swali la tatu na la nne yenye vipengele **vitatu (3)** kila moja na swali la tano na la sita yenye vipengele **viwili (2)** kila moja. Mtahiniwa atatakiwa kujibu vipengele vyote kwa kuandika majibu mafupi. Kila kipengele kitakuwa na alama **mbili (2)** na hivyo, kufanya jumla ya alama **20**.

**Sehemu C** itakuwa na swali **moja (1)** lenye vipengele **vitano (5)** ambapo mtahiniwa atatakiwa kutafsiri picha/ramani/mchoro na kujibu dhana mbalimbali za kijiografia. Sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **kumi (10).**

## 5.0 UMAHIRI UTAKAOTAHINIWA

Umahiri utakaotahiniwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi ni kama ifuatavyo:

5.1 Kutunza mazingira ya jamii inayomzunguka, kutunza kumbukumbu za matukio ya kihistoria na kutumia elimu ya hali ya hewa katika shughuli za kila siku;

5.2 Kudumisha utamaduni wa mtanzania, kujenga uhusiano mwema kwa jamii inayomzunguka na kuthamini mashujaa wetu;

5.3 Kutumia ramani katika mazingira na kufahamu mfumo wa jua;

5.4 Kuthamini na kulinda rasimali za nchi, kutambua shughuli za uzalishaji mali katika jamii, kutumia stadi za ujasiliamali na shughuli za kila siku;

5.5 Kujenga tabia ya usafi wa mwili, kutunza mavazi katika kudumisha usafi na kutunza mazingira katika kudumisha makazi safi;

5.6 Kutambua kanuni zinazohitajika katika mapishi, kutayarisha vyakula aina tofauti na kutengeneza vinywaji tofauti;

5.7 Kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji, kutengeneza picha zenye ujumbe tofauti kwa jamii, kubuni chapa mbalimbali za sanaa za ufundi, kufinyanga maumbo mbalimbali na kutengeneza vitu kwa kutumia makunzi mbalimbali; na

5.8 Kujenga utayari wa kujifunza, kutafuta masoko ya bidhaa ndogo ndogo, na kutumia kanuni za usimamizi wa fedha.

**Jedwali la Utahini Somo la 03 Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi**

| Na. | UMAHIRI MAHUSUSI | NGAZI ZA NYANJA YA UTAMBUZI ZITAKAZOPIMWA | | | | | | Idadi ya Vipengele vya Maswali kwa kila Umahiri | Asilimia ya uzito kwa kila Umahiri |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kukumbuka | Kuelewa | Kutumia | Kuchambua | Kutathmini | Kuunda | | |
| 1. | Kutunza mazingira ya jamii inayomzunguka; kutunza kumbukumbu za matukio ya kihistoria; na kutumia elimu ya hali ya hewa katika shughuli za kila siku. | | | | | | | 9 | 25.7 |
| 2. | Kudumisha utamaduni wa mtanzania; kujenga uhusiano mwema kwa jamii inayomzunguka; na kuthamini mashujaa wetu. | | | | | | | 8 | 22.9 |
| 3. | Kutumia ramani katika mazingira na kufahamu mfumo wa jua. | | | | | | | 5 | 14.2 |
| 4. | Kuthamini na kulinda rasimali za nchi; kutambua shughuli za uzalishaji mali katika jamii; kutumia stadi za ujasiliamali na shughuli za kila siku. | | | | | | | 7 | 20.0 |
| 5. | Kujenga tabia ya usafi wa mwili; kutunza mavazi katika kudumisha usafi; na kutunza mazingira katika kudumisha makazi safi. | | | | | | | 2 | 5.7 |
| 6. | Kutambua kanuni zinazohitajika katika mapishi; kutayarisha vyakula aina | | | | | | | 2 | 5.7 |

| Na. | UMAHIRI MAHUSUSI | NGAZI ZA NYANJA YA UTAMBUZI ZITAKAZOPIMWA | | | | | | Idadi ya Vipengele vya Maswali kwa kila Umahiri | Asilimia ya uzito kwa kila Umahiri |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kukumbuka | Kuelewa | Kutumia | Kuchambua | Kutathmini | Kuunda | | |
| | tofauti; na kutengeneza vinywaji tofauti. | | | | | | | | |
| 7. | Kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji; kutengeneza picha zenye ujumbe tofauti kwa jamii; kubuni chapa mbalimbali za sanaa za ufundi; kufinyanga maumbo mbalimbali; na kutengeneza vitu kwa kutumia makunzi mbalimbali. | | | | | | | 1 | 2.9 |
| 8. | Kujenga utayari wa kujifunza; kutafuta masoko ya bidhaa ndogo ndogo; na kutumia kanuni za usimamizi wa fedha. | | | | | | | 1 | 2.9 |
| **Idadi ya Vipengele vya Maswali kwa kila Ngazi** | | | | | | | | **35** | |
| **Asilimia ya Uzito wa Vipengele vya Maswali kwa kila Ngazi ya Utambuzi** | | | | | | | | | **100** |

## 04 HISABATI

### 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya Mtihani wa Hisabati imeandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa mwaka 2015 ulioanza kutumika 2017 (toleo la 2019). Maswali ya mtihani wa Hisabati yatatokana na malengo ya mwanafunzi yaliyowekwa katika Muhtasari wa somo la Hisabati kwa shule za msingi kuanzia Darasa la III hadi la VII wa mwaka 2019. Aidha, umahiri uliotajwa katika muhtasari wa mwaka 2019 ndio utakaotahiniwa ili kubaini umahiri aliopata mwanafunzi katika miaka saba ya elimu ya msingi.

Fomati hii ni zao la maboresho yaliyofanyika kutoka fomati ya mwaka 2020 ambayo ilikuwa na maswali **45**. Fomati iliyoboreshwa ina maswali **nane (8)** yenye jumla ya vipengele **33** ambayo yametoka katika aina zote **nane (8)** za umahiri mahususi zilizotokana na umahiri mkuu wa aina tatu. Lengo la maboresho haya ni kumwezesha mtahiniwa kuendana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia yanayotokea duniani kote na ujenzi wa msingi wa umahiri katika masomo ya sekondari na elimu ya juu.

### 2.0 MALENGO YA JUMLA

Mtihani wa Hisabati unalenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika:

2.1 Kujenga uwezo wa kufikiri kimantiki kwa mwanafunzi;

2.2 Kujenga udadisi na uwezo wa utatuzi wa matatizo;

2.3 Kuweka misingi muhimu ya matumizi ya teknolojia, mawasiliano, ufikiri na tafakuri;

2.4 Kujenga uwezo wa kuchambua na kuwasilisha taarifa;

2.5 Kukuza uelewa wa maumbo, vipimo na matumizi yake katika maisha; na

2.6 Kujenga uwezo wa kujiamini katika kutumia maarifa, stadi na mwelekeo wa kihisabati katika maisha ya kila siku.

## 3.0 UMAHIRI MKUU

Mtihani huu unalenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika:

3.1 Kutumia lugha ya kihisabati kuwasilisha wazo au hoja katika maisha ya kila siku;

3.2 Kufikiri na kuhakiki katika maisha ya kila siku; na

3.3 Kutatua matatizo katika mazingira tofauti.

## 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

Mtihani wa somo la Hisabati utakuwa na karatasi **moja (1)** na utafanyika kwa muda wa **saa 2:00** kwa watahiniwa wote isipokuwa watahiniwa wenye mahitaji maalum ambapo mtihani wao utafanyika kwa **saa 2:40**. Mtihani utakuwa na sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **nane (8)** yenye vipengele **33**. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali yote yenye jumla ya alama **50**.

**Sehemu A** itakuwa na swali **moja (1)** ambalo ni swali la kwanza lenye vipengele **10** kutoka katika Umahiri Mahususi wa Matendo ya Kihisabati. Kila kipengele kitakuwa na alama **moja (1)** na hivyo, jumla ya alama katika sehemu hii zitakuwa **10**.

**Sehemu B** itakuwa na maswali **matano (5)**; swali la pili, la tatu, la nne, la tano na la sita yenye jumla ya vipengele **18** vya mafumbo (Word Problems) kutoka kwenye umahiri mahususi wa aina **tano (5)**. Swali la pili litakuwa na vipengele **sita (6)** kila kipengele alama **moja (1)**, swali la tatu, la nne, la tano na la sita yatakuwa na vipengele **vitatu (3)** kila moja na kila kipengele kitakuwa na alama **mbili (2)**. Hivyo, jumla ya alama katika sehemu hii itakuwa **30**.

**Sehemu C** itakuwa na maswali **mawili (2)**, swali la saba na la nane. Swali la saba litakuwa na vipengele **viwili (2)** kutoka katika Umahiri Mahsusi wa kutumia stadi za takwimu kuwasilisha taarifa mbalimbali na swali la nane litakuwa na vipengele **vitatu (3)** kutoka katika umahiri wa kutumia stadi za maumbo katika miktadha ya Hisabati. Kila kipengele kitakuwa na alama **mbili (2)**, hivyo kufanya jumla ya alama katika sehemu hii kuwa **10**.

## 5.0 UMAHIRI MAHUSUSI UTAKAOPIMWA

Umahiri mahususi utakaopimwa katika mtihahi huu ni kama ifuatavyo:

5.1 kutumia dhana ya namba kuwasiliana katika mazingira tofauti;

5.2 kutumia stadi za mpangilio kufumbua mafumbo katika maisha ya kila siku;

5.3 kutumia matendo ya namba ya kihisabati katika kutatua matatizo;

5.4 kutumia stadi ya uhusiano wa namba na vitu katika miktadha mbalimbali;

5.5 kutumia stadi za vipimo katika miktadha mbalimbali;

5.6 kutumia stadi za maumbo katika miktadha ya Hisabati;

5.7 kutumia stadi za aljebra katika maisha ya kila siku; na

5.8 kutumia stadi za takwimu kuwasilisha taarifa mbalimbali.

**Jedwali la Utahini Somo la 04 Hisabati**

| Na. | UMAHIRI MAHUSUSI | NGAZI ZA NYANJA YA UTAMBUZI ZITAKAZOPIMWA | | | | | | Idadi ya Vipengele vya Maswali kwa kila Umahiri | Asilimia ya uzito kwa kila Umahiri |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kukumbuka | Kuelewa | Kutumia | Kuchambua | Kutathmini | Kuunda | | |
| 1. | Kutumia dhana ya namba kuwasiliana katika mazingira tofauti. | | | | | | | 6 | 18.18 |
| 2. | Kutumia stadi za mpangilio kufumbua mafumbo katika maisha ya kila siku. | | | | | | | 3 | 9.09 |
| 3. | Kutumia matendo ya namba ya kihisabati katika kutatua matatizo. | | | | | | | 10 | 30.30 |
| 4. | Kutumia stadi ya uhusiano wa namba na vitu katika miktadha mbalimbali. | | | | | | | 3 | 9.09 |
| 5. | Kutumia stadi za vipimo katika miktadha mbalimbali. | | | | | | | 3 | 9.09 |
| 6. | Kutumia stadi za maumbo katika miktadha ya Hisabati. | | | | | | | 3 | 9.09 |
| 7. | Kutumia stadi za aljebra katika maisha ya kila siku. | | | | | | | 3 | 9.09 |
| 8. | Kutumia stadi za takwimu kuwasilisha taarifa mbalimbali. | | | | | | | 2 | 6.07 |
| **Idadi ya Vipengele vya Maswali kwa kila Ngazi** | | | | | | | | **33** | **100** |
| **Asilimia ya Uzito wa Vipengele vya Maswali kwa kila Ngazi ya Utambuzi** | | | | | | | | | |

## 05 SAYANSI NA TEKNOLOJIA

### 1.0 UTANGULIZI

Fomati ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi katika somo la Sayansi na Teknolojia imeandaliwa kwa kuzingatia Muhtasari wa somo hilo wa mwaka 2015 ulioanza kutumika 2017 (toleo la 2019). Muhtasari huo umebainisha Umahiri Mkuu na Umahiri Mahsusi ambao mwanafunzi anatakiwa kuupata katika ngazi ya Elimu ya Msingi Darasa la III hadi VII. Hivyo, mtihani wa somo la Sayansi na Teknolojia utakaoandaliwa kwa kutumia fomati hii, utalenga kupima umahiri alioupata mtahiniwa kuanzia Darasa la III hadi VII.

Fomati hii ni zao la maboresho yaliyofanyika kutoka fomati ya mwaka 2020 ambayo ilikuwa na maswali **45**. Hivyo, mtihani wa somo la Sayansi na Teknolojia utakuwa maswali **nane (8)** yenye jumla ya vipengele **35** kutoka katika umahiri mahususi wa aina **tisa (9)** uliotokana na umahiri mkuu wa aina **tatu (3)**. Lengo la maboresho haya ni kumwezesha mtahiniwa kuendana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia yanayotokea duniani kote na ujenzi wa msingi wa umahiri katika masomo ya sekondari na elimu ya juu.

### 2.0 MALENGO YA JUMLA

Mtihani wa somo la Sayansi na Teknolojia unalenga kupima ni kwa kiwango gani mtahiniwa anaweza:

2.1 Kukuza uelewa na kutumia maarifa, stadi na kuwa na mwelekeo wa kisayansi na teknolojia;

2.2 Kujenga uwezo wa kutumia sayansi na teknolojia katika kutatua matatizo katika maisha ya kila siku; na

2.3 Kukuza stadi za kutenda na kutumia vifaa mbalimbali vya teknolojia.

### 3.0 UMAHIRI MKUU

Mtihani utazingatia tathmini ya ujuzi na utendaji wa mtahiniwa katika:

3.1 Kufanya uchunguzi na ugunduzi wa kisayansi na kiteknolojia;
3.2 Kufahamu Misingi ya Sayansi na Teknolojia; na
3.3 Kutunza afya na mazingira.

## 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

Mtihani wa somo la Sayansi na Teknolojia utakuwa na karatasi **moja (1)** na utafanyika kwa muda wa **saa 1:30** kwa watahiniwa wote isipokuwa, kwa watahiniwa wenye mahitaji maalum ambapo mtihani wao utafanyika kwa **saa 1:45**. Mtihani utakuwa na sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **nane (8)** yenye vipengele **35**. Mtihani wa somo la Sayansi na Teknolojia utakuwa na jumla ya alama **50**.

**Sehemu A** itakuwa na maswali **matatu (3);** swali la kwanza, la pili na la tatu yenye jumla ya vipengele **20**. Swali la kwanza litakuwa na vipengele **10** vya maswali ya kuchagua herufi ya jibu sahihi kati ya machaguo matano **(A-E)** aliyopewa. Swali la pili litakuwa na vipengele **vitano (5)** ambavyo vitamtaka mtahiniwa kuoanisha maswali yaliyopo katika **Orodha A** na majibu yaliyopo katika **Orodha B**. Swali la tatu litakuwa na vipengele **vitano (5)** ambavyo vitamtaka mtahiniwa kukamilisha sentensi kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi. Kila kipengele kitakuwa na alama **moja (1)** na hivyo, kufanya jumla ya alama katika sehemu hii kuwa **20**.

**Sehemu B** itakuwa na maswali **matatu (3)**, swali la nne na swali la tano yenye vipengele **vitatu (3)** kwa kila swali na swali la sita lenye vipengele **vinne (4)**. Maswali yote katika sehemu hii yatakuwa ya kuandika majibu mafupi. Kila kipengele kitakuwa na alama **mbili (2)** na hivyo, kufanya jumla ya alama katika sehemu hii kuwa **20**.

**Sehemu C** itakuwa na maswali **mawili (2)**; swali la saba na la nane. Swali la saba litakuwa na vipengele **vitatu (3)** na swali la nane litakuwa na vipengele **viwili (2)**. Maswali hayo yatahusisha picha/ michoro au dhana mbalimbali za kisayansi zinazopima stadi za kukokotoa. Kila kipengele kitakuwa na alama **mbili (2)**. Hivyo kufanya jumla ya alama katika sehemu hii kuwa **10**.

## 5.0 UMAHIRI UTAKAOTAHINIWA

Umahiri utakaotahiniwa katika mtihani wa somo la Sayansi na Teknolojia ni kama ifuatavyo:

5.1 kuchunguza vitu vilivyopo katika mazingira;

5.2 kutambua aina anuai za nishati na matumizi yake;

5.3 kutambua nadharia za kisayansi na kiteknolojia;

5.4 kutumia TEHAMA;

5.5 kumudu stadi za kisayansi;

5.6 kufanya majaribio kwa usahihi;
5.7 kufuata kanuni za usafi ili kuwa na afya na mazingira bora;
5.8 kufuata kanuni za afya ili kujenga afya bora; na
5.9 kutambua mifumo mbalimbali ya mwili wa binadamu.

**Jedwali la Utahini Somo la 05 Sayansi na Teknolojia**

| **Na.** | **UMAHIRI MAHUSUSI** | **NGAZI ZA NYANJA YA UTAMBUZI ZITAKAZOPIMWA** | | | | | | **Idadi ya Vipengele vya Maswali kwa kila Umahiri** | **Asilimia ya uzito kwa kila Umahiri** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Kukumbuka** | **Kuelewa** | **Kutumia** | **Kuchambua** | **Kutathmini** | **Kuunda** | | |
| 1. | Kuchunguza vitu vilipo katika mazingira. | | | | | | | 4 | 11.4 |
| 2. | Kutambua aina anuai za nishati na matumizi yake. | | | | | | | 4 | 11.4 |
| 3. | Kutambua nadharia za kisayansi na kiteknolojia. | | | | | | | 4 | 11.4 |
| 4. | Kutumia TEHAMA. | | | | | | | 4 | 11.4 |
| 5. | Kumudu stadi za Kisayansi. | | | | | | | 3 | 8.6 |
| 6. | Kufanya majaribio kwa usahihi. | | | | | | | 4 | 11.4 |
| 7. | Kufuata kanuni za usafi ili kuwa na afya na mazingira bora. | | | | | | | 3 | 8.6 |
| 8. | Kufuata kanuni za afya ili kujenga afya bora. | | | | | | | 4 | 11.4 |
| 9. | Kutambua mifumo mbalimbali ya mwili wa binadamu. | | | | | | | 5 | 14.4 |
| **Idadi ya Vipengele vya Maswali kwa kila Ngazi** | | | | | | | | **35** | **100** |
| **Asilimia ya Uzito wa Vipengele vya Maswali kwa kila Ngazi ya Utambuzi** | | | | | | | | | |

## 06 URAIA NA MAADILI

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi somo la Uraia na Maadili inazingatia Muhtasari wa somo la Uraia na Maadili Elimu ya Msingi Darasa la III-VII wa mwaka 2015 ulioanza kutumika 2017 (toleo la 2019). Muhtasari huu unasisitiza ujenzi wa umahiri kwa mwanafunzi, ili kuishi katika maadili yanayokubalika na jamii. Pia, muhtasari umejikita katika kumjengea mwanafunzi tabia inayokubalika ya kuheshimu na kuithamini jamii, uwajibikaji, ustahimilivu, uadilifu pamoja na kudumisha amani.

Fomati hii ni zao la maboresho yaliyofanyika kutoka fomati ya mwaka 2020 ambayo ilikuwa na maswali **45**. Hivyo, mtihani wa somo la Uraia na Maadili utakuwa na maswali **sita (6)** yenye jumla ya vipengele **35** kutoka katika umahiri mahususi wa aina **ishirini (20)** uliotokana na umahiri mkuu wa aina **sita (6)**. Lengo ni kumwezesha mtahiniwa kumaliza Elimu ya Msingi akiwa na umahiri zaidi wa kufikiri, kuchambua mambo na kutumia maarifa aliyoyapata katika mazingira yanayomzunguka ili aweze kuendana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia yanayotokea duniani kote na ujenzi wa msingi wa umahiri katika masomo ya sekondari na elimu ya juu.

## 2.0 MALENGO YA JUMLA

Mtihani utapima ni kwa kiwango gani mtahiniwa anaweza:

2.1 Kuelewa asasi na taasisi za kisiasa na kijamii na kazi zake katika utawala wa kidemokrasia;

2.2 Kutafisiri, kuthamini na kuheshimu vitambulisho vya taifa letu, Katiba, muundo na uendeshaji wa Serikali;

2.3 Kuelewa misingi ya kidemokrasia katika shughuli za utawala na uongozi;

2.4 Kutambua wajibu wao, kuheshimu na kutetea haki za binadamu na usawa wa sheria;

2.5 Kuelewa na kushiriki katika shughuli za utawala, uongozi, ulinzi na usalama wa taifa katika jamii wanamoishi;

2.6 Kuwa wabunifu na kuweza kubaini na kuchambua matatizo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii na kubuni mbinu za kuyatatua;

2.7 Kutambua tofauti baina ya watu zitokanazo na itikadi na hali zao na kujenga uvumilivu kuhusu tofauti hizo;

2.8 Kujenga moyo wa umoja wa kitaifa na ushirikiano baina ya jamii za Tanzania na jamii za mataifa mengine; na

2.9 Kuishi kwa kutumia Elimu ya masuala mtambuka.

## 3.0 UMAHIRI MKUU

Utahini kwa kutumia fomati hii utazingatia upimaji wa ujuzi na utendaji wa mtahiniwa katika:

3.1 Kuheshimu jamii;

3.2 Kuithamini jamii;

3.3 Kuwa mwajibikaji;

3.4 Kuwa mstahimilivu;

3.5 Kuwa mwadilifu; na

3.6 Kudumisha amani na maelewano.

## 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

Mtihani wa somo la Uraia na Maadili utakuwa na karatasi **moja (1)** na utafanyika kwa muda wa **saa 1:30** kwa watahiniwa wote isipokuwa, kwa watahiniwa wenye mahitaji maalum ambapo utafanyika kwa **saa 1:45**. Mtihani utakuwa na sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **sita (6)** yenye vipengele **35**. Watahiniwa watatakiwa kujibu maswali **yote** katika kila sehemu. Mtihani huu utakuwa na jumla ya alama **50**.

**Sehemu A** itakuwa na maswali **matatu (3)**; Swali la kwanza, la pili na la tatu yenye jumla ya vipengele **20**. Swali la kwanza litakuwa na vipengele **10** vya Kuchagua jibu sahihi kati ya machaguo **matano (5) A-E**. Kila kipengele kitakuwa na alama **moja (1)**, hivyo, kufanya jumla ya alama **10**. Swali la pili litakuwa la kuoanisha lenye vipengele **vitano (5)**. Kila kipengele kitakuwa na alama **moja (1)**, hivyo, kufanya jumla ya alama **tano (5)**. Swali la tatu litakuwa na vipengele **vitano (5)** vya kujaza nafasi iliyoachwa wazi. Kila kipengele kitakuwa na alama **moja (1)** na hivyo kufanya jumla ya alama **tano (5)**. Hivyo, sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **20**.

**Sehemu B** itakuwa na maswali **mawili (2)**; swali la nne na la tano yenye vipengele **vitano (5)** kila moja. Swali la nne litakuwa na vipengele **vitano (5)** vya kukamilisha jedwali/mchoro au kupanga

sentensi ili kuleta mantiki. Kila kipengele kitakuwa na alama **mbili (2)** na hivyo kufanya jumla ya alama **10**. Swali la tano litakuwa na vipengele **vitano (5)** vya majibu mafupi. Kila kipengele kitakuwa na alama **mbili (2)** na hivyo kuwa na jumla ya alama **10**. Hivyo, sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **20**.

**Sehemu C** itakuwa na swali **moja (1)** lenye vipengele **vitano (5)** vya kutafsiri picha/ramani, kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali yatakayoulizwa kwa kuandika majibu mafupi au kuandika maelezo mafupi juu ya dhana au hoja. Kila kipengele kitakuwa na alama **mbili (2)**. Hivyo, sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **10**.

## 5.0 UMAHIRI UTAKAOTAHINIWA

Umahiri utakaopimwa katika mtihani wa somo la Uraia na Maadili ni kama ifuatavyo:

5.1 Kujipenda na kuwapenda watu wengine, kuipenda na kujivunia shule yake, na kupenda Tanzania kwa kuenzi tunu za nchi na asili yake;

5.2 Kujijali na kuwajali wengine, kutunza mazingira na kujenga uhusiano mwema na watu wengine katika jamii;

5.3 Kulinda rasilimali na maslahi ya nchi, kusimamia majukumu yanayomhusu nyumbani na shuleni, kutii sheria na kanuni katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku, kuwa na nidhamu na kushirikiana katika kutekeleza majukumu ya nyumbani na shuleni;

5.4 Kuvumilia katika maisha ya kila siku, kufikia malengo aliyojiwekea kwa kuwa na mtizamo chanya na kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu;

5.5 Kuaminika katika jamii, kutimiza majukumu yake kwa uwazi na ukweli na kusimamia haki; na

5.6 Kuchangamana na watu wenye asili tofauti, kuheshimu tofauti za kiutamaduni na mitazamo miongoni mwa watu wa jamii tofauti na kujenga urafiki mwema na mataifa mengine.

**Jedwali la Kutahini somo la 06 Uraia na Maadili**

| Na. | UMAHIRI MAHUSUSI | NGAZI ZA NYANJA YA UTAMBUZI ZITAKAZOPIMWA | | | | | | Idadi ya Vipengele Vya Maswali kwa kila Umahiri | Uzito % Kwa Asilimia Kwa Kila Umahiri |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kukumbuka | Kuelewa | Kutumia | Kuchambua | Kutathmini | Kuunda | | |
| 1. | Kujipenda na kuwapenda watu wengine; kuipenda na kujivunia shule yake; na kupenda Tanzania kwa kuenzi tunu za nchi na asili yake. | | | | | | | 5 | 14.3 |
| 2. | Kujijali na kuwajali wengine; kutunza mazingira; na kujenga uhusiano mwema na watu wengine katika jamii. | | | | | | | 5 | 14.3 |
| 3. | Kulinda rasilimali na maslahi ya nchi; kusimamia majukumu yanayomhusu nyumbani na shuleni; kutii sheria na kanuni katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku; kuwa na nidhamu; na kushirikiana katika kutekeleza majukumu ya nyumbani na shuleni. | | | | | | | 10 | 28.5 |
| 4. | Kuvumilia katika maisha ya kila siku; kufikia malengo aliyojiwekea kwa kuwa na mtizamo chanya; na kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu. | | | | | | | 5 | 14.3 |

| Na. | UMAHIRI MAHUSUSI | NGAZI ZA NYANJA YA UTAMBUZI ZITAKAZOPIMWA | | | | | | Idadi ya Vipengele Vya Maswali kwa kila Umahiri | Uzito % Kwa Asilimia Kwa Kila Umahiri |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kukumbuka | Kuelewa | Kutumia | Kuchambua | Kutathmini | Kuunda | | |
| 5. | Kuaminika katika jamii; kutimiza majukumu yake kwa uwazi na ukweli; na kusimamia haki; na | | | | | | | | |
| 6. | Kuchangamana na watu wenye asili tofauti; kuheshimu tofauti za kiutamaduni na mitazamo miongoni mwa watu wa jamii tofauti; na kujenga urafiki mwema na mataifa mengine. | | | | | | | 5 | 14.3 |
| **Idadi ya Vipengele vya Maswali kwa kila Ngazi** | | | | | | | | **35** | |
| **Asilimia ya Uzito wa Vipengele vya Maswali kwa kila Ngazi ya Utambuzi** | | | | | | | | | **100** |